TOLEO LA MESSENGER LA **TURATHI ZISIZOGUSIKA**

United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization

KITENGO CHA TURATHI ZISIZOGUSIKA
www.unesco.org/culture/ich

AGOSTI 2007 n° 7
ISSN 2071-7784





## Maafikiano 2003

KUIDHINISHWA NA MATAIFA KUFIKIA JUNI 4, 2007

1 ALGERIA
2 MAURITIUS
3 UJAPANI
4 GABON
5 PANAMA
6 UCHINA
7 JAMHURI YA AFRIKA YA KATI
8 LATVIA
9 LITHUANIA
10 BELARUS
11 JAMHURI YA KOREA
12 USHELISHELI
13 JAMHURI YA KIARABU YA SYRIA
14 UMOJA WA MILKI ZA KIARABU
15 MALI
16 MONGOLIA
17 CROATIA
18 MISRI
19 OMAN
20 DOMINICA
21 HINDI
22 VIET NAM
23 PERU
24 PAKISTANI
25 BHUTAN
26 NIGERIA
27 ICELAND
28 MEXICO
29 SENEGAL
30 ROMANIA
31 ESTONIA
32 LUXEMBOURG
33 NICARAGUA
34 CYPRUS
35 UHABESHI
36 BOLIVIA
37 BRAZIL
38 BULGARIA
39 HUNGARY
40 JAMHURI YA KIISLAMU YA IRAN
41 JAMHURI YA MOLDOVA
42 YORDANI
43 SLOVAKIA
44 UBELGIJI
45 UTURUKI
46 BUKINI
47 ALBANIA
48 ZAMBIA
49 ARMENIA
50 ZIMBABWE
51 CAMBODIA
52 JAMHURI YA YUGOSLAV YA MAKEDONIA YA AWALI
53 MOROCCO
54 UFARANSA
55 CÔTE D'IVOIRE
56 BURKINA FASO
57 TUNISIA
58 HONDURAS
59 SAO TOME AND PRINCIPE
60 ARGENTINA
61 UFILIPINO
62 BURUNDI
63 PARAGUAY
64 JAMHURI YA DOMINICA
65 GUATEMALA
66 HISPANIA
67 KYRGYZSTAN
68 MAURITANIA
69 UGIRIKI
70 LEBANON
71 NORWAY
72 AZERBAIJAN
73 URUGUAY
74 SAINT LUCIA
75 COSTA RICA
76 VENEZUELA
77 NIGER
78 CUBA
79 MONACO

# Kamati Maalumu kati ya Serikali za Mataifa Wanachama Yakutana Chengdu

Tarehe 23 Mei, 2007 Kamati maalumu kati ya serikali za Mataifa Wanachama ya kulinda Turathi za Tamaduni Zisizogusika ilifanya kikao chake cha kwanza kisichokuwa cha kawaida Chengdu, ambao ni mji mkuu wa jimbo la Sichuan, Uchina. Mkutano huo ulioandaliwa vizuri, ulifuatiwa na matukio kadha yaliyougeuza mji wa Chengdu kuwa mji mkuu wa turathi zisizogusika wa ulimwengu. Mkutano huo ulishughulikia maswala tata ambayo ni muhimu kwa utekelezaji wa Maafikiano. Mojawapo ni kutayarisha vigezo vya kuandikwa kwa vito vya turathi kwenye orodha mbili za Maafikiano ambazo ni Orodha Wakilishi ya Turathi za Tamaduni Zisizogusika za Kibinadamu na Orodha ya Turathi za Tamaduni Zisizogusika inayohitaji Ulinzi wa Haraka. Kulikuwa na majadiliano ya utangulizi juu ya maswala mengine, kwa mfano, orodha hizi zitahusiana vipi? Kito cha turathi kinaweza kuandikwa katika orodha zote mbili kwa wakati mmoja? Kuna uwezekano wa kuhamisha kito kutoka katika orodha moja hadi nyingine iwapo kuna haja? Je, maumbo yaliyoandikwa katika orodha yanaweza kubakia huko daima au kwa muda?

Kikao cha Chengdu pia kilijadili juu ya usaidizi wa kitaaluma. Kamati itategemea sana utaalamu wa kienyeji, kitaifa, kimataifa, mashirika yasiyokuwa ya serikali na watu binafsi ndani na nje ya jamii za mila husika. Huko Chengdu, Kamati iliteua vigezo vitakavyoiruhusu kuteua rasmi mashirika yasiyokuwa ya serikali ili kutoa usaidizi. Kadhalika, itachunguza upya ushirikiano kati yake na mashirika hayo. Vigezo hivi vinasisitiza umilisi wa mashirika hayo katika mawanda ya Turathi za Tamaduni Zisizogusika, na kadhalika ukubalifu wao wa malengo na kiini cha Maafikiano hasa katika kushirikiana na jamii pamoja na makundi

*(yaendelea uk. 2)*



© Culture Department of Chengdu Municipality

*Ufunguzi wa Kikao na Mhe. Bw. Sun Jiazheng, Waziri wa Utamaduni wa Jamhuri ya Watu ya Uchina (wa nne kutoka kulia), Mhe.Bw.Jiang Jufeng,Gavana wa Jimbo la Sichuan (wa tatu kutoka kulia) na Mhe. Bw.Zhang Xinsheng, Mwenyekiti wa Halmashauri Kuu ya UNESCO na Naibu wa Waziri wa Elimu (wa tatu kutoka kushoto).*

## Tahariri

Sekta ya Turathi za Tamaduni Zisizogusika inaendelea kutumikia matawi ya Maafikiano ya 2003: baada ya kikao cha kawaida (Juni) na kisicho cha kawaida (mapema Novemba) ambavyo ni vikao vya Mkutano Mkuu wa Mataifa Wanachama, mwaka wa 2006 ulikamilishwa na kikao cha kwanza cha kawaida cha Kamati maalumu kati ya serikali za Mataifa Wanachama (katikati ya Novemba).

Kufuatia kikao kisichokuwa cha kawaida cha Kamati mjini Chengdu mwishoni mwa Mei 2007, ambacho pia kiliandaliwa kwa ujuzi mkubwa na mamlaka za Uchina, Kamati itakutana tena kwenye kikao chake cha pili cha kawaida (Septemba 3-7) huko Tokyo kupitia mwaliko wa serikali ya Ujapani. Toleo hili la *Messenger* lina ripoti za kina kuhusu mkutano wa Chengdu.

Lengo kuu la mikutano ya mwaka huu ni kuibuka na Maongozi mengi ya Utendakazi ili kutekeleza Maafikiano. Maongozi hayo ambayo yanatayarishwa yanalenga kurekodiwa kwa vito vya turathi zisizogusika kwenye Orodha za Maafikiano pamoja na taratibu zingine husika; uteuzi wa programu, miradi na shughuli mbalimbali ili kupata usaidizi wa kimataifa; na matumizi ya Hazina ya Turathi za Tamaduni Zisizogusika. Maswala haya yatakapojadiliwa na kuamuliwa na Mkutano Mkuu, Maafikiano yataweza kutekelezwa kikamilifu. Hii inamaanisha kwamba Kamati inaweza kutumia Hazina hiyo, kwa mfano, katika kutoa kibali cha usaidizi wa kimataifa, kurekodi vito kwenye Orodha na kuteua programu na shughuli ambazo zinaweza kuakisi vyema malengo ya Maafikiano. Kikao kingine cha Mkutano Mkuu kimepangwa kufanyika Juni 2008.

Tuonane Tokyo!

*Rieks Smeets, Kitengo cha Turathi Zisizogusika*




*Kamati maalumu kati ya Serikali za Mataifa Wanachama wakati wa ufunguzi wa Kikao cha Kwanza kisichokuwa cha kawaida Chengdu, Uchina.*

*(yaendelea toka uk. 1)* mbalimbali. Hata hivyo, majukumu ya mashirika hayo na uhusika wa jamii na wawakilishi wa jamii hizo katika utekelezaji wa Maafikiano yatajadiliwa zaidi katika kikao cha Tokyo.

Kamati pia iliamua kwamba nembo ilihitajika ili kuunga mkono na kuendeleza Maafikiano. Nembo itasaidia kuweka Maafikiano hayo wazi- kama ilivyo katika makubaliano na mipango mingine mingi ya UNESCO. Katika kikao kijacho cha Kamati huko Tokyo, jopo la utendakazi huenda likaundwa ili kupanga mashindano ya wazi katika kuchora nembo hiyo. Tutaripoti haya katika toleo lijalo la *Messenger*.

Kipengele kingine cha ajenda kilihusu kuwekwa kwa masimulizi, mila na maumbo ya kitamaduni, ambayo yalitangazwa kuwa Vito vya Thamani vya Mapokezi ya Mdomo na Turathi za Zisizogusika za Kibinadamu kwenye Orodha Wakilishi. Mambo kadha yalifafanuliwa, hususan haki na masharti ya kuwekwa kwa Vito hivyo kutoka kwa nchi ambazo bado hazijaidhinisha Maafikiano.

Mambo mengine ya ajenda yalihusu kukubaliwa kwa watazamaji kwenye vikao vya Kamati na taratibu za Hazina ya Kulinda Turathi za Tamaduni Zisizogusika. Kamati ilizingatia umuhimu wa Kifungu cha 18 cha Maafikiano ambacho kinakubali kuteuliwa na kuendelezwa kwa miradi, mipango na shughuli za kitaifa, kijimbo na kieneo, ambayo yatajihusisha na malengo ya Maafikiano. Maswala haya yote yalizua mijadala ya kusisimua ambayo pia ilibainisha tofauti za maoni kutoka kwa mataifa hasa matarajio na mielekeo yao dhidi ya turathi za tamaduni zisizogusika na Maafikiano kwa jumla. Kutokana na ujuzi na weledi wa afisi ya rais ya Uchina, makubaliano yalifikiwa katika maswala mengi na mwongozo wa manufaa ukatolewa kwa maswala mengine. Hili litaiwezesha Afisi ya Utawala kutayarisha hati za utendakazi za mkutano ujao ambao pia utawasilisha rasimu zingine za Maongozi ya Utendakazi ili kujadiliwa na Kamati.

# Vigezo vya kuandika turathi zisizogusika kwenye Orodha za Maafikiano

Kamati maalumu kati ya serikali za Mataifa Wanachama ilitekeleza mojawapo ya mambo muhimu: kufafanua vigezo vya kuandika turathi zisizogusika kwenye Orodha Wakilishi na Orodha ya Ulinzi wa Haraka. Hili lilifuata kipindi cha mashauriano na majadiliano ambayo yalianza na mikutano kadha ya wataalamu iliyoandaliwa na Afisi ya Utawala kabla ya Maafikiano kuanza kufanya kazi tarehe 20 Aprili 2006. Mkutano wa kwanza ulijadili "Vigezo vya kuandika vito kwenye Orodha vilivyowekwa na Maafikiano ya 2003," ambao uliandaliwa na UNESCO tarehe 5 na 6 Disemba 2005 huko Paris. Mkutano wa pili "Uhusika wa jamii katika kuhifadhi Turathi za Tamaduni Zisizogusika ambao uliandaliwa na Kituo cha Utamaduni kwa UNESCO (ACCU) cha Asia/Pacific. Mkutano huu ulifanyika Tokyo tarehe 13 hadi 15 Machi 2006.

Katika kikao cha kawaida (tarehe 27-29 Juni 2006) cha Mkutano Mkuu wa Mataifa Wanachama wa Maafikiano, wito ulitolewa kwa Kamati kuandaa vigezo vitakavyotumiwa kuandika turathi kwenye Orodha zile mbili. Kamati ilijadili jambo hili katika kikao chake cha kwanza Algiers (tarehe 18- 19 Novemba 2006). Mjadala wa awali ulifuatiwa na kipindi cha Mataifa Wanachama kupeleka, kwa njia ya maandishi, maoni yao; Mataifa 32 yaliitikia mwito huu yakatoa maoni kuhusu muundo wa Orodha hizo, vigezo vya kuandika na taratibu za uteuzi na uandishi. UNESCO iliitikia mwaliko wa Serikali ya Hindi na kuandaa "Mkutano wa wataalamu wa Orodha zilizoanzishwa kulingana na Maafikiano ya 2003" huko New Delhi (tarehe 2-4 Aprili 2007). Wataalamu walipitia rasimu iliyofanyiwa marekebisho ya vigezo vya Orodha Wakilishi pamoja na vigezo vipya vilivyotayarishwa vya Orodha ya Ulinzi wa Haraka. Wataalamu hao walitoa mapendekezo kadha ambayo Afisi ya Utawala iliona yalisaidia kutayarisha rasimu ya vigezo ambayo ilichunguzwa na Kamati huko Chengdu.

Huko Chengdu pia, Kamati ilishughulikia vigezo vya Orodha ya Ulinzi wa Haraka kabla ya kushughulikia Orodha Wakilishi. Vigezo vyote katika Orodha zote mbili vilifanana. Hata hivyo, kigezo cha pili na cha sita cha Orodha ya Ulinzi wa Haraka vinagusia hali ya ulinzi wa haraka (au ulinzi wa haraka sana kama ulivyofafanuliwa katika Kifungu cha 17.3 cha Maafikiano) na taratibu za kushauriana na Mataifa Wanachama katika hali inayohitaji ulinzi wa haraka zaidi. Kwa upande mwingine, kigezo cha pili cha Orodha Wakilishi kinasema kwamba vito vilivyopendekezwa lazima vitosheleze malengo ya Orodha Wakilishi kama inavyoelezwa katika Kigungu cha 16. Kulingana na kigezo cha kwanza – ambacho kinafanana katika Orodha zote mbili – kito kitakachoteuliwa lazima kitosheleze maana ya turathi za tamaduni zisizogusika kama inavyoeleweka kwenye Maafikiano. Fomu fafanuzi ya kutuma maombi itayaeleza Mataifa Wanachama yanayoteua jinsi yatakavyoonyesha kwamba kito fulani kinatosheleza maana hiyo.

Wanachama wa Kamati walikumbusha pia kuhusu mjadala wa maana za istilahi mbalimbali zilizotumiwa katika Maafikiano, huku baadhi ya wanachama wakipendekeza kufanywe marudio ya faharasa za Turathi za Tamaduni Zisizogusika ambazo zilichapishwa awali katika mwezi wa Juni 2002. Hata hivyo, wanachama wengine walionelea kwamba Kamati inahitaji kuzingatia utekelezwaji wa Maafikiano, na kwamba kazi ya kushughulikia upya maana za istilahi ionekane kama shughuli inayoendelea. Kigezo cha tatu ambacho kinajihusisha na hatua za kulinda pia kinafanana katika Orodha zote mbili. Wanachama walikubaliana na maoni yaliyotolewa na wataalamu waliokutana New Delhi kwamba hata vito imara vinavyoandikwa katika Orodha Wakilishi pia vinahitaji mpango wa uongozi wa uendeshaji, hasa katika kubainisha baadhi ya hatari zinazofungamana na mfanyiko wenyewe wa uandikaji katika orodha. Mpango madhubuti wa kuhifadhi ungewekwa hususan kwa vito vinavyoandikwa kwenye Orodha ya Ulinzi wa Haraka (ambavyo vinahatarishwa) badala ya vile vilivyo katika Orodha Wakilishi.

Kigezo cha nne (kinachofanana katika Orodha zote) kinashughulikia kushiriki na

© Culture Department of Chengdu Municipality




*Mhe. Bw. Wang Xuexian (Uchina), Mwenyekiti wa kikao cha Kamati huko Chengdu.*

© Culture Department of Chengdu Municipality


中国成都国际非物质文化遗产节

非遗节

开场锣鼓敲起来

听 八旬翁敲金钱板 千年琴奏续梁音

那一刻 "非遗"是没有国界的语言

免费金沙遗址门票 明天可以去领了

提醒市民：首期未中奖者可以继续报名参与

古蔺肝苏：培育中药国际市场竞争力


成都商报

"非遗"狂欢 成都亮出国际文化品牌

50余国代表共商"非遗"保护大计

成都端出"非遗"视觉盛宴

*Baadhi ya yaliyochapishwa kwenye vyombo vya habari uhusu sherehe ya kwanza ya Turathi za Tamaduni Zisizogusika (tazama ukurasa 4).*

kukubali kwa jamii, kundi au watu binafsi. Wanachama wa Kamati walikubaliana kwamba kushiriki kikamilifu kwa wale wanaohusika na kito cha turathi ni muhimu hasa katika kutayarisha uteuzi wa kito na kutekelezwa kwa hatua za ulinzi baadaye. Huku wakikubali kanuni inayohitaji ukubalifu huru wa jamii unaotokana na ufahamu wa yanayotendeka, wanachama walisisitiza kwamba haina haja ya kuwa na utaratibu mahsusi wa kufuatwa katika kukubali huko. Hii ni kwa sababu sheria na desturi za tamaduni tofauti zitakuwa na nguvu katika kuamua utoaji wa kibali kwa njia tofauti tofauti, kwani tamaduni na sheria za mataifa pia hutofautiana.

Kwa vile Mataifa Wanachama na Kamati watakuwa wamepata tajriba kulingana na wakati, kanuni au taratibu za jinsi ya kutoa vibali huenda zikaibuka zenyewe, na Kamati huenda ikatoa mwongozo kwa Mataifa yanayoteua vito kuhusu namna ya kuonyesha ukubalifu wao. Wanachama walijikumbusha kuwa kila Taifa Mwanachama linahitaji kuweka hesabu yake na masharti yatakayozingatiwa katika kurekodiwa kwa vito kwenye hesabu hiyo – kiini cha kigezo cha tano ambacho kinafanana katika Orodha zote mbili – kinaweza kuyahamasisha mataifa kutimiza jukumu hili. Wanachama wa Kamati pia walijikumbusha kuwa mahesabu hayo ni kazi zinazoendelea ambazo "zitatayarishwa na kurejelewa upya kila mara" kwa kurejelea maneno ya Maafikiano. Kigezo hiki hakitarajii kwamba hesabu inaweza kukamilika katika wakati wowote ule.

Uzingativu wa Kamati katika mfanyiko wa uteuzi na kurekodiwa kwa vito hauishii katika kufuata vigezo hivi. Katika kikao chake cha pili Tokyo mwezi wa Septemba 2007, Kamati itajadili rasimu ya Maongozi ya Utendakazi huku ikiainisha taratibu zitakazofuatwa, ratiba ya kutayarishwa na kuchunguzwa kwa maombi, pamoja na muundo utakaotumiwa na wateuzi. Huku yakijumuisha vigezo vilivyokubaliwa Chengdu, Maongozi ya Utendakazi yatawasilishwa katika kikao cha pili cha Mkutano Mkuu mwezi wa Juni, 2008.

## Orodha Wakilishi ya Turathi za Tamaduni Zisizogusika za Binadamu

Katika majadiliano ya uteuzi ambayo yatazingatia muundo utakaotolewa na Kamati, Taifa Mwanachama litaomba kuonyesha kwamba kito kilichopendekezwa kurekodiwa katika Orodha Wakilishi kinatosheleza vigezo vifuatavyo:

R.1. Kito kinahusisha turathi za tamaduni zisizogusika kama inavyoelezwa katika Kifungu cha 2 cha Maafikiano ya kuhifadhi turathi za tamaduni zisizogusika.

R.2. Kurekodiwa kwa kito kutapelekea kujulikana, kutambuliwa kwa umuhimu wa turathi za tamaduni zisizogusika, pamoja na usemezo, hivyo kuonyesha uanuwai wa tamaduni ulimwenguni na kuthibitisha usanii wa binadamu.

R.3. Hatua za ulinzi zinafafanuliwa ili kulinda na kuhimili kito.

R.4. Kito kimeteuliwa baada ya kushirikishwa kikamilifu kwa jamii husika, kundi, au ikiwezekana, watu binafsi ambao watakuwa wametoa kibali kwanjia huru na kwa ufahamu wao.

R.5. Kito kimewekwa katika hesabu ya turathi za tamaduni zisizogusika zilizoko katika eneo la Taifa Mwanachama.

## Orodha ya Turathi za Tamaduni Zisizogusika Zinazohitaji Ulinzi wa Haraka

Katika majadiliano ya uteuzi ambayo yatazingatia muundo utakaotolewa na Kamati, Taifa Mwanachama litaomba kuonyesha kwamba kito kilichopendekezwa kurekodiwa katika Orodha Zinazohitaji Ulinzi wa Haraka kinatosheleza vigezo vifuatavyo:

U.1. Kito kinahusisha turathi za tamaduni zisizogusika kama inavyoelezwa katika Kifungu cha 2 cha Maafikiano ya kuhifadhi turathi za tamaduni zisizogusika.

U.2. a) Kito kinahitaji ulinzi wa haraka kwa sababu kuwepo kwakekunahatarishwa hata baada ya juhudi za jamii husika, kundi, au ikiwezekana, watu binafsi na Taifa au Mataifa Wanachama husika.

(au)

b) Kito kinahitaji ulinzi wa haraka sana kwa sababu kimekabiliwa na vitisho hivi kwamba hakiwezi kudumu bila ya ulinzi wa haraka.

U.3. hatua za kulinda zinafafanuliwa ili kuiwezesha jamii husika, kundi, au ikiwezekana, watu binafsi kuendeleza desturi na mapokezi ya kito hicho.

U.4. Kito kimeteuliwa baada ya kushirikishwa kikamilifu kwa jamii husika, kundi, au ikiwezekana, watu binafsi ambao watakuwa wametoa kibali kwa njia huru na kwa ufahamu wao.

U.5. Kito kimewekwa katika hesabu ya turathi za tamaduni zisizogusika zilizoko katika eneo la Taifa Mwanachama.

U.6. Katika hali za haraka zaidi, Taifa Mwanachama husika limeshirikishwa katika kurekodiwa kwa kito kulingana na Kifungu cha 17.3 cha Maafikiano.

MCHAPISHAJI Idara ya Turathi za Tamaduni Zisizogusika (ITH)
Sekta ya Tamaduni, UNESCO
1 Rue Miollis
75732 Paris Cedex 15, Ufaransa
Barua pepe: ich@unesco.org
Kipepesi: +33 (0) 145685752
MHARIRI MKUU Rieks Smeets
JOPO LA UHARIRI Estelle Blaschke, Jana Gough, Fleur Perrier, Frank Proschan, David Stehl
MWANA-RUWAZA Jean-Luc Thierry

***Toleo la Messenger kuhusu Turathi Zisizogusika*** linapatikana katika umbo la chapa na elektroniki kwa Kiingereza, Kifaransa, Kihispania na Kiarabu.

Nakala ya Kiarabu imewezeshwa kupitia kwa mchango wa kifedha wa Mamlaka ya Utamaduni na Turathi ya Abu Dhabi, Milki ya Abu Dhabi – U.A.E.

Yote yaliyomo yanaweza kupakuliwa katika (www.unesco.org/culture/ich) na kupigwa chapa bila malipo ilimradi mwandishi atambuliwe.


© Conselho das Aldeias Wajãpi-Apina


turathi zisizogusika

## Kuwatambulisha Vijana Kuhusu Turathi Zisizogusika


Turathi za tamaduni zisizogusika ni nini na kwa nini tunasema “hai”? Kwa nini ni muhimu kwa jamii na watu ulimwenguni kote? Hupatikana katika maumbo gani, huigizwa kwa njia gani na hupokezwa vipi? Hukabiliwa na vitisho gani? Ni kwa jinsi gani UNESCO inajaribu kuzilinda na kwa nini tunahitaji mkataba? Haya ni baadhi ya maswali ya vijana wa leo ambao yanahitaji kushughulikiwa.

UNESCO inafanya bidii kubwa kudumisha mkataba wa Turathi Zisizogusika ili kukuza utambuzi wa kuweko na pia umuhimu wa turathi za tamaduni zisizogusika. Turathi hizi zinaweza tu kulindwa ikiwa kizazi cha sasa kina haja na kimehamasishwa kuendeleza mila zao. Kufikia sasa Shirika hili halijatayarisha vifaa vyovyote ambavyo vinawatambulisha watoto juu ya Turathi za Tamaduni Zisizogusika na kueleza kwa nini zinahitaji kulindwa. Hali hii itabadilika kupitia chapisho la UNESCO liitwalo *Tell Me About….Living Heritage*, ambacho ni kitabu kinacholenga watoto wa umri wa miaka 8-12. Kitabu hicho kinawakaribisha watoto kuvumbua utajiri anuwai wa turathi za tamaduni Zisizogusika. Wasomaji wachanga watavumbua mifano ya michoro ya Turathi za Tamaduni Zisizogusika kutoka ulimwenguni na watajifunza historia ya Maafikiano ya 2003. Aidha, watajifunza programu za UNESCO kuhusu mipango ya ulinzi. Matoleo ya Kiingereza, Kifaransa na Kihispania yatachapishwa mwaka wa 2007.

Kitabu kingine kinachoeneza turathi zisizogusika kwa watu kimechapishwa hivi karibuni na kituo cha utamaduni cha Asia/ Pacific kwa UNESCO (ACCU) kiitwacho *Animal in Asia tradition- Intangible Cultural Heritage Around us* (Wanyama katika mila za watu wa Asia- Turathi za Tamaduni Zisizogusika miongoni mwetu). Kitabu hiki kinaeleza mila za turathi ziishizo na masimulizi kutoka katika maeneo yote ya Asia ambapo nyoka, tumbili, ndovu na simba hutekeleza jukumu muhimu. Kinajumuisha takriban mapokezi 30 mbalimbali tokea vikagarosi na maigizo ya densi hadi katika sherehe zinazohusisha ndovu halisi, vinyago, maleba na upakaji wa rangi mwilini, mapambo, vikaragosi na ala za muziki. Haya ni baadhi ya vito katika mila hizi. Kitabu hicho ambacho kinafaa kutumiwa na watoto tokea vidato vya chini ni cha kwanza katika msururu wa vitabu vitatu. ACCU inaendeleza juhudi za kutafsiri kitabu hiki katika lugha mbalimbali ndani na nje ya eneo la Asia.



© UNESCO



© Asia/Pacific Cultural Centre for UNESCO (ACCU)

Kwa habari zaidi, tafadhali enda kwa: http://www.accu.or.jp/ich/en/materials/materials1.html


© Culture Department of Chengdu Municipality

*Wageni katika maonyesho ya picha “Turathi-hai: Kuchunguza Zisizogusika”.*

## Turathi-Hai: “Kuchunguza Zisizogusika”. Maonyesho ya picha yanasafiri

Baada ya Paris (Ufaransa) na Abu Dhabi (Umoja wa Milki za Kiarabu), maonyesho ya picha “Turathi-hai: Kuchunguza Zisizogusika” yalisafiri hadi Chengdu (Uchina) katika kikao cha kwanza kisichokuwa cha kawaida cha Kamati maalumu kati ya Serikali za Mataifa Wanachama. Kama sehemu ya Sherehe ya Turathi za Tamaduni Zisizogusika ambazo zilipangwa na kuhimiliwa na Manispaa ya Chengdu, maonyesho hayo yalitandaza takriban zaidi ya picha 100 za maumbo ya Turathi za Tamaduni Zisizogusika kote ulimwenguni- mengi yakiwa vito vya Masimulizi vya mapokezi ya mdomo na Turathi Zisizogusika za Kibinadamu- pamoja na maonyesho ya picha zilizobainisha zaidi ya mifano 500 ya Turathi za Tamaduni Zisizogusika zilizoorodheshwa katika hesabu za kitaifa za Uchina.

Sherehe hiyo ambayo iliandaa mchezo na mawasilisho, ilifanyika kuanzia tarehe 23 Mei hadi tarehe 10 Juni, 2007 na kujumuisha idadi kubwa ya wageni pamoja na kuenezwa katika vyombo vya habari.

Maonyesho hayo sasa yanasafiri kuenda Afrika ambapo yataonyeshwa Addis Ababa wakati Uhabeshi itakapokuwa ikisherehekea milenia yake mwanzoni mwa Septemba 2007. Kwa kuangazia Turathi za Tamaduni Zisizogusika barani Afrika, maonyesho hayo yatafanyika ndani na nje ya Makao Makuu ya Tume ya Uchina kwa Afrika (*Economic Commission for Africa (ECA)*